

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**MKOA WA KILIMANJARO**

Anwani ya Simu: "REGCOM KILIMANJARO"

Simu Na: 027-2754236/7

Nukushi Na. 027-2753248/027-2751381

Barua pepe E-mail: [ras@kilimanjaro.go.tz](mailto:ras@kilimanjaro.go.tz)

[ras.kilimanjaro@tamisemi.go.tz](mailto:ras.kilimanjaro@tamisemi.go.tz)



OFISI YA MKUU WA MKOA

S.L.P 3070,

MOSHI.

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Tarehe 25 Oktoba, 2019 nilifanya ziara ya kikazi katika shamba la Lambo Estate lililopo Wilayani Hai.

Lengo la ziara hiyo lilikuwa kusikiliza tena utatuzi wa malalamiko ya waliokuwa wafanyakazi wa shamba hilo ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakiomba ruhusa ya kufanya shughuli za kilimo katika shamba hilo ambalo ni mali ya Vyama vya Ushirika vya Foo, Nronga na Machame Wari.

Baada ya ziara hiyo na kuwasikiliza wanachi, viongozi wa wilaya ya Hai pamoja na wadau wengine wa maendeleo ndani ya mkoa wa Kilimanjaro, napenda kuutangazia umma mambo yafuatayo nikiwa na Mkuu wa Wilaya pamoja na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya pamoja kamati ya ulinzi na usala ya mkoa:-


1. Jumla ya kaya **65** zilizomo ndani ya shamba la Lambo Estate zipewe ekari 2 kila kaya moja ambazo ni sawa na jumla ya ekari **130** ili wazitumie kwa ajili ya kilimo cha kujikimu kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2019/2020 na ugawaji huo utafanyika kila mwaka hadi hapo utaratibu wa uendeshaji wa shamba utakapokamilika.
2. Jumla ya ekari **26** kati ya **156** ambazo zitabaki baada ya mgao wa ekari 2 kwa kila kaya, zilimwe na kaya hizo **65** kama shamba lao la ushirika hadi hapo utaratibu wa uendeshaji wa shamba utakapokamilika.
3. Nimevunja Bodi ya Ushirika inayosimamia shamba la Lambo Estate ambayo inajumuisha Vyama vya Msingi vitatu vinavyomiliki shamba hilo kwa kushindwa kuendeleza. Nimemuagiza mrajiis wa vyama vya ushirika kuteua bodi ya mpito kutoka miongoni mwa viongozi wa vyama vya msingi

vinavyomiliki Lambo Estate, kuendesha chama hadi mkutano mkuu utakapo kaa kufanya uchaguzi wa viongozi wa kudumu.

4. Kuhusu sehemu ya shamba kukodishwa ekari **656** kwa kampuni ya EPK; nimeagiza kusitishwa kwa mchakato huo mpaka utakapopatikana ushahidi wa kuridhisha juu ya uwepo wa kampuni hiyo inayotaka kuingia mkataba wa uendeshaji wa sehemu ya shamba hilo kwa ekari **656**.

Aidha, natumia fursa hii kuwataka wataalam wa ushirika ngazi ya mkoa na wilaya kufuata taratibu za kisheria ili kuhakikisha maelekezo haya yanatekelezwa.

Imetolewa na:-

  
Dkt. Anna E. Mghwira  
**MKUU WA MKOA**  
**KILIMANJARO**  
13/11/2019